

## JIHADHARI NA DUNIA

*I.K. Ndyanabo*

Mwana nakuelezea, maadili yasikia  
Rohoni uyawekea, kwa dhati nakuusia  
Shika ukizingatia, maishani saidia  
Ee mwana nakukanya, jihadhari na dunia.

Hima amka haraka, wasia nakuachia  
Dunia hii viraka, vyashika na kuachia  
Kila kitu kama paka, kamata na kuachia  
Ee mwana nisikia, jihadhari na dunia.

Dunia ninakusihi, yazusha na kuzuzua  
Usije kuona fihi, kwa hivyo vipya tambua  
Pokea hizi nasihi, ushike takufalia  
Ee mwana nakuasa, jihadhari na dunia.

Ikizuka shikamana, ina tabia dunia  
Vingi visivyo mana, takuvutia kwa nia  
Chini utaandamana, pasipo kujitwania  
Ee mwana nakuomba, jihadhari na dunia.

Wasia ninakupasha, binadamu heshimia  
Madhara kujiepusha, kwa wote hao jamia  
Wa Mtwara na Arusha, maovu sije pamia  
Ee mwana jiepusha, jihadhari na dunia.

Vilema na masikini, waja wa Mola sawia  
Wa Tabora, Kurasini, ni watu wa jumuwia  
Uwaweke heshimani, heshima sije vulia  
Ee mwana upendoni, jihadhari na dunia.

Watu mwiko kuhunia, hauna tija uhuni  
Kazi zako kazania, pasipo kuwarubuni  
Taifa tajivunia, kaziyo yenye thamani  
Ee mwana shikilia, jehadhari na dunia.

Uonevu ondolea, mbaya nakuapia  
Wanyonge sionelea, wana haki nao pia  
Mwana utaendelea, mema ukiwalipia  
Ee mwana timizia, jihadhari na dunia.

Mwanangu namalizia, mzazio heshimia  
Uwezalo fanyizia, malipo yatatimia  
Kama si hapa dunia, ahera tapata mia  
Mwanangu shika wasia, mzazio naachia.

I.K.NDYANABO (Yangu Macho)

S.L.P. 873

TABORA.